




MAELEZO NA MASHARTI YA USHIRIKI.



**ZABUNI YA KUNUNUA KIWANJA NAMBA 190 BLOCK 22
KIBADA, KIGAMBONI DAR-ES-SALAAM.**

WAKALA WA :

**The Chief Executive Officer
WAT-Human Settlements Trust
Plot 5, Block 37, Kawawa Road
P.O Box 31606
Dar es Salaam,**

1.0 Utangulizi.

Sisi Capital Shelterworks Limited tumeteuliwa kama wakala wa mmiliki mali tajwa hapo juu kutafuta wateja wenye uhitaji wa kununua Kiwanja husika kwa njia ya tenda.

2.0 Sifa za kushiriki.

Mchakato wa kuuza mali hizi uko wazi kwa mtu Binafsi, Mashirika ya Kijamii , vyama vya Ushirika , makampuni binafsi ya ndani na nje ya nchi , mashirika ya Umma ambao hawazuiwi na sheria yoyote kutojihusisha na kuingia mikataba kwa sababu ya ubadhirifu au uhalifu Kulingana na sheria za kimataifa au nchini walipo.

Makampuni ya nje, au watu binafsi kutoka nje ya nchi watatakiwa kuwa wamekamilisha masharti ya uwekezaji kulingana na matakwa ya Sheria chini ya Tanzania Investment Center.

3.0 Utambulisho na taarifa muhimu zinazotakiwa

- a. Jina Kamili la (Mtu Binafsi), au Jina Kamili la Makundi Ya Kijamii k.m Sacco's , Vikundi Vya Ushirika, Kampuni Binasfi au Mashirika ya Umma.
- b. Kitambulisho na Uthibitisho wa Uraia wa mtu binafsi.
- c. Anuani Kamili (Sanduku la Posta, ,Fax,E-mail)
- d. Kama (Makundi Ya Kijamii k.m Sacco's, Vikundi vya Ushirika), Kampuni Binafsi au za nje, Shirika la Umma ambatanisha :-
 - uthibitisho wa Usajili, mahali na tarehe ya Kusajiliwa
 - mahali ilipo ofisi na anuani ya mahali pa kufanyia kazi
 - an authenticated copy of the certificfate of incorporation.
 - Certified true copy of the Memorandum and Articles of association
 - Tanzania Investment Center (TIC) Certificate
 - majina (jina) na anuani ya wana hisa pamoja na nakala iliyothibitishwa ya share certificates.
 - majina ya subsidiary companies.
 - jina la mwakilishi atakaye husika na taratibu za kisheria hadi kufikia kuhamisha mali (Simu ,Sanduku la Posta, ,Fax,E-mail n.k)
 - jina la benki inayotunza pesa pamoja na Namba ya Akaunti
 - Malipo yote yatafanywa kwa kutumia Shilingi za kitanzania au Dolar za. Kimarekani

4 .0 Dhamana ya Malipo :

Mwombaji ataandika kiasi alichokuwa tayari kununua Kiwanja halafu atalipa asilimia 20 % ya bei aliyopendekeza kwenye benki ya muuzaji.

Jina la Benki: National Microfinance Bank (NMB)

Tawi: Bank House

Namba ya Akaunti: 20103500456

Jina la Akaunti: WAT – HUMAN SETTLEMENTS TRUST

Bank pay-in slip iambatanishwe pamoja na barua ya maombi ndani ya bahasha iliyofungwa kwa lakili.

Malipo haya ya awali yatatumika kama dhamana ya kumalizia malipo na hayatarudishwa kwa yoyote ambaye baada ya kuarifiwa kukubaliwa maombi yake/ yao watashindwa kumalizia malipo ndani ya siku ishirini na moja tokea tarehe ya kuarifiwa hivyo.

Ambao Hawatafanikiwa , pesa yao itarudishwa kwa njia hiyo waliyolipia na kwa anuani kama ilivyo tolewa katika kifungu **d(risasi ya tisa)** hapo juu.

5 **Uwasilishi**

Maombi yawasilishwe ndani ya bahasha iliyofungwa na lakili na juu yake yaandikwe maneno yafuatayo

“Maombi ya kununua Kiwanja Na190, Block 22 Kibada, Kigamboni.”

Na yatumwe kwa:

WAT-HUMAN SETTLEMENTS TRUST (WAT-HST),
Kinondoni, Plot No. 5, Block 37,
Kawawa Road, Kinondoni,
P.O. Box 31606, Dar es salaam,
TANZANIA. (Ofisi inatizamana na Open University of Tanzania,
Kinondoni).

6 **Gharama Za Uhamisho** wa Milki ni juu ya Mnunuzi.

7 **Angalizo** WAT-HST haitawajibika kuuza Kiwanja hiki kwa Bei itakayoonekana kuwa ya juu na haitalazimika kutoa sababu za kutofanya hivyo.

8 **Mwisho:** Muda wa kuwasilisha maombi ni saa **10. 00** alasiri Ijumaa **20 Julai 2018.**

90. Maelezo ya Kiwanja

Kiwanja hiki kinamilikiwa chini ya hati milki ya Ardhi Namba127344 ya miaka 99 tokea Aprili 2008.

Kiwanja hiki cha WAT-HST kiko Kibada maeneo ya Kigamboni, umbali wa kilometa 23.7 tokea mwanzo wa Daraja la Mwalimu Nyerere –Kurasini. Mahali pamepangwa kwa aajili ya Makazi. Maendeleo ya sasa ni pamoja na Nyumba za kisasa za mradi wa NSSF Kigamboni.

Eneo linafaaa sana kujenga Maduka makubwa ya kisasa au majumba ya kukaa (apartments).

Sehemu hii inafikika kirahisi kwa kuwa kando ya Barabara iliyojengwa ya lami tokea Magogoni Ferry kuelekea Mbagala.

Namna ya Kufika; Kutumia Uber ingiza Kigamboni Bridge kwa kuanza Safari halafu mwisho wa safari **Nhendes Pub** geuka mkono wa Kushoto eneo wazi ndipo kilipo Kiwanja husika (fuata Barabara ya Bluu)

-6,9096614, 39.340561N

